



## Yote kuhusu Kondomu ya kike ya FC2



**Kwa tendo la kujamiiana  
lenye furaha na salama**



## Yote Kuhusu

### Kondomu ya kike ya FC2

## Kwa tendo la kujamiiana lenye furaha na salama

Unapoongea na watu kuhusu kondomu ya kike ya FC2 kwa mara ya kwanza, mara nyingi huwa na maswali mengi juu yake. Na wanapoanza kutumia FC2, wanaweza kuwa na maswali mengi zaidi. Chapisho hili linakupa majibu ya maswali yote hayo. Ili kukusaidia kupata majibu sahihi kwa urahisi tumeigawanya katika sehemu zifuatazo:

1. Taarifa za FC2
2. Watumiaji wa FC2
3. Uingizwaji wa FC2
4. FC2 wakati wa tendo la kujamiiana
5. FC2 pamoja na njia nyingine za kuzuia mimba
6. Jinsi ya kutumia kondomu ya kike ya FC2



## Taarifa za FC2

### Kondomu ya kike ya FC2 ni nini?

FC2 ni kondomu laini, nyororo na ngumu, iliyotengenezwa kwa nyenzo ya mpira, ambayo huvaliwa ndani ya uke. Ni ya wazi ambayo ina urefu wa sentimita 17 au inchi 6.5, ina pete ya ndani inayoweza kutanuka na pete ya nje iliyoviringishwa. Pete ya ndani, upande uliofungwa wa kondomu, hutumiwa kuingiza FC2. Pia inashikilia kondomu wakati wa kujamiiana. Pete kubwa ya nje, sehemu ya wazi ya kondomu, inabaki nje ya uke.

- FC2 huingia sambamba na uke na kuziba shingo ya kizazi. Inashikilia shahawa baada ya kumwaga, huzuia ujauzito usiotarajiwa, na huweka kizuizi cha virusi na bakteria ambao husababisha magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU.
- FC2 pia hutoa kinga ya ziada dhidi ya magonjwa ya zinaa kwa kufunika viungo vya nje vya mwanamke na sehemu ya chini ya uume.

### Je! FC2 ni salama?

- Vipimo vimeonyesha kwamba FC2 ni njia salama na madhubuti ya kuzuia mimba zisizotarajiwa na magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU.
- FC2 ni njia madhubuti kama zilivyo njia nyingine za kuzuia endapo itatumika kwa usahihi na mfululizo.
- Kila kondomu ya kike ya FC2 inapimwa kielektroniki kuhakikisha ubora.
- FC2 imejaribiwa kwa ISO 10993 ambayo ni pamoja na vipimo vya biocompatibility, cytotoxicity (tendo la uharibifu kwenye seli fulani), mutagenicity (husababisha mabadiliko ya seli), kuwasha na systemic toxicity (athari mbaya za viungo vya mwili na tishu).
- Kondomu ya kike ya FC2 hufikia viwango vya hali ya juu vya ubora vilivyowekwa na mashirika ya afya ya kimataifa kama FDA na WHO.

## Kwanini tunapaswa kutumia FC2?

---

Kuna sababu nyingi za kufurahisha na za kupendeza za kutumia FC2. Hapa kuna baadhi ya sababu hizo!

- FFC2 ina njia mbili za ulinzi. Hii inamaanisha inatoa kinga dhidi ya ujauzito na magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU. FC2 inaruhusu wanawake na wanaume kujamiiana kwa amani bila hofu ya matokeo mabaya.
- FC2 inaweza kuingizwa kabla ya kujamiiana. Hii inamaanisha hauhitaji kuvuruga maandalizi ya awali kabla ya kujamiiana ili kuvaa kondomu.
- FC2 imeundwa kutoshea ndani ya uke na inaruhusu uume kuingia kwa uhuru ndani ya kondomu wakati wa kujamiiana.
- FC2 inabadilika haraka kulingana na joto la mwili kwa hivyo inahisi joto na asili.
- FC2 imewekwa vilainishi. Ukipenda, unaweza kuongeza mafuta zaidi au kilainishi jamii ya maji kwa ndani ya kondomu au nje ya kondomu au moja kwa moja kwenye uume. Hii inaweza kurahisisha uingiaji na kuruhusu uume kuingia na kutoka kwa urahisi wakati wa kujamiiana.
- FC2 haina aleji na ni chaguo zuri kwa wanaume na wanawake ambao wana aleji ya mpira.
- Uume huitaji kuwa umesimama ili utumie FC2, na sio lazima uondolewe mara tu baada ya kujamiiana.
- Wanaume na wanawake wanaweza kufurahia kwa pamoja wakiingiza FC2. Pete zile mbili pia zinaweza kuongeza raha wakati wa kujamiiana. Wanaume wengine wanafurahia kuigusa pete ya ndani ya kondomu, wakati wanawake wanaweza kufurahia hisia za pete ya nje kugusa kisimi chao..

## Je! FC2 inahitaji hali maalum ya uhifadhi?

---

FC2 haizoroti kwenye hali ya joto la juu au unyevu hivyo hazihitaji hali maalum ya uhifadhi.

## Je! FC2 inapatikana katika ukubwa tofauti?

---

Hapana, FC2 inawatosha wanawake wote bila kujali ukubwa wao au maumbile yao.

### **Kwanini FC2 ina muonekano tofauti na kondomu ya kiume?**

---

FC2 imeundwa kutoshea ndani ya uke sambamba na kuta za uke, na inaruhusu uume kuingia kwa uhuru wakati wa kujamiiana. Pia hutoa kinga ya ziada dhidi ya magonjwa ya zinaa kwa kufunika viungo vya nje vya mwanamke na sehemu ya chini ya uume.

### **Ni aina gani ya vilainishi vinaweza kutumika na FC2?**

---

FC2 imewekwa vilainishi maalum. Unaweza kuongeza mafuta zaidi au kilainishi jamii ya maji aidha kwa ndani ya kondomu au nje ya kondomu au moja kwa moja kwenye uume.



## 2 Watumiaji wa FC2

### Nani anaweza kutumia FC2?

---

FC2 ni njia nzuri, yenye furaha na salama kwa wanawake na wanaume ambao wanashiriki tendo la kujamiiana. FC2 inaweza kutumiwa na:

- Wanaume na wanawake ambao wana aleji na mpira
- Wanawake walio katika hedhi
- Wanawake wajawazito
- Wanawake ambao wamejifungua karibuni
- Wanawake ambao wanakaribia au wamepita menopause
- Wanawake ambao wamefanyiwa upasuaji kutoa uterasi

### Ni kwanini FC2 inapaswa kupatikana kwa wanawake?

---

Katika maeneo mengi, wanawake wana nafasi ndogo au hawana kabisa uamuzi kwenye maswala ya kujamiiana na hawako katika nafasi ya kuwaomba wenzi wao wasijamiane na watu wengine au kujadili matumizi ya kondomu ya kiume. Kondomu ya kike kwa sasa ndiyo njia pekee inayoweza kutumiwa na wanawake wenyewe kutoa kinga mara mbili dhidi ya magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU, na ujauzito usiopangwa. FC2, kwa hivyo, inachangia udhibiti binafsi wa wanawake na uwezesaji na huongeza maarifa yao juu ya miili yao. FC2 husaidia kuboresha mawasiliano kati ya wanaume na wanawake.

### Je! FC2 inaweza kutumika kwa watu ambao wana aleji na mpira aina ya latex?

---

FC2 inatengenezwa kutokana na nitrile polymer ambazo ni nyenzo maalum ambazo zimepimwa kikamilifu na kuonekana hazina aleji. Ni chaguo zuri kwa wanaume na wanawake ambao wana aleji na mpira aina ya latex.

### Je! FC2 inaweza kutumika wakati wa ujauzito?

---

Ni salama kabisa kutumia FC2 unapokuwa mjamzito.

### **Je! FC2 inaweza kutumika wakati wa hedhi? ?**

---

FC2 inaweza kutumika wakati wa hedhi lakini unaweza kutaka kuiingiza kabla ya kujamiiana na kuiondoa mapema baadaye kwani haitazuia kutoka kwa hedhi.

### **Je! FC2 inaweza kutumika mapema kiasi gani baada ya kujifungua?**

---

FC2 inaweza kutumika mara tu unapohisi uko tayari kujamiiana baada ya kujifungua. Inaweza kuwa chaguo bora wakati huu wakati njia zingine za kuzuia mimba hazifai.

### **Je! FC2 inaweza kutumika kwa kujamiiana kinyume na maumbile?**

---

Hakuna utafiti juu ya ufanisi wa FC2 kwa matumizi ya kujamiiana kinyume na maumbile na haijaidhinishwa kwa matumizi ya kujamiiana kinyume na maumbile. Hata hivyo, mashirika mengi ya afya ya umma yanahamasisha FC2 kwa kujamiiana kinyume na maumbile. Asasi hizi hushauri kuingiza FC2 ndani ya sehemu ya haja kubwa na kuondoa pete ya ndani kabla ya kujamiiana kinyume na maumbile. Inawezekana kwanza kuondoa pete ya ndani na kisha kuweka kondomu juu ya uume uliosimama. Wanaume wengine huweka pete juu ya uume ili ibane ipasavyo.

### **Je! FC2 inaweza kutumika endapo mwanaume ana uume mrefu kuliko uume wa kawaida?**

---

FC2 imejaribiwa katika tafiti nyingi za kliniki kwa nchi kadhaa na asili za kikabila. Imegundulika kuwa FC2 inaweza kutumika kwa maumbo na saizi zote za wanaume na wanawake.

# 3

## Uingizwaji wa FC2

### Je FC2 ni rahisi kutumiwa?

---

Kama kitu chochote kipya, inahitaji mazoezi kidogo lakini kumbuka mazoezi huboresha. Jaribu FC2 angalau mara 3. Tafuta mkao wa starehe. Hii inaweza kuwa kusimama, kukaa, kuchuchumaa au kulala chini. Mshirika yeyote anaweza kuingiza FC2. Furahia kuingiza ndani!

### Je! FC2 iingizwe muda gani?

---

FC2 inaweza kuingizwa aidha masaa machache au mara tu kabla ya kujamiiana na sio lazima itolewe mara tu baada ya kujamiiana.

### Je! Utajuaje kama FC2 imeingizwa kwa usahihi?

---

Unaweza kuhisi endapo imekaa vizuri. Pete ya nje inapaswa kulala wima karibu na sehemu ya mwanzoni mwa uke. FC2 inapaswa kuwa imelazwa vizuri dhidi ya ukuta wa uke.

### Je! FC2 inaweza kupotelea mwilini?

---

Hapana. FC2 haiwezi kupotelea ndani ya mwili. FC2 inaziba shindo la kizazi na shingo ya kizazi chako ni ndogo sana kiasi kwamba haiwezekani FC2 kupenya eneo hili. Shingo ya kizazi hufunguka wakati wa kujifungua pekee.

### Nifanye nini ikiwa pete ya ndani haijaka vizuri?

---

- Toa kondomu ya kike.
- lingize tena kondomu ya kike. Ijaribu tena katika nafasi tofauti. Unaweza kuiweka ukiwa umesimama, umekaa, umechuchumaa au umelala chini.

### Nifanyeje endapo kondomu ya kike itaniponyoka mikononi wakati wa kuingiza?

---

Futa vidole vyako kwenye tishu ili kuondoa kilainishi kilichozidi na endelea kuingiza kondomu ya kike.





### **Je! FC2 itatoa bikra?**

---

Kuna uwezekano kwamba FC2 itatoa bikra wakati wa kuingiza?

### **Je! Unaweza kukojoa wakati FC2 imeingizwa?**

---

Ndio, unaweza kukojoa wakati FC2 imeingizwa. Hakikisha pete ya nje haizibi tundu la mkojo. Endapo itahitajika Sukuma pete ya nje nyuma kidogo kabla haujakojoa. Jisafishe baada ya hapo na hakikisha pete ya nje imewekwa vizuri kabla ya kujamiiana.

# 4

## FC2 wakati wa tendo la kujamiiana

### Je ni kweli kwamba FC2 inaweza kuongeza raha wakati wa kujamiiana?

---

Ndio. Baadhi ya wanaume wanaona kugusa pete ya ndani wakati wa kujamiiana inaongeza hamu. Wanawake wengine wanapenda hali ya pete ya nje kusugua kisimi chao. Mshirika yeyote anaweza kuingiza FC2 ambayo inaweza kuongeza furaha. Nyenzo zilizotumika pia ni laini na nyororo na hubadilika haraka kufuatia joto la mwili, na kusababisha tendo la kujamiiana kuwa la asili.

### Je! Pete ya ndani inasikika vipi wakati wa kujamiiana?

---

Wanawake wengi na wanaume wanasema pete ya ndani inawaongezea raha wakati wa kujamiiana. Endapo pete ya ndani haijaka vizuri, jaribu kuiweka sawa au kuitoa na kuingiza tena.

### Je! Kuna ulazima wa kushika pete ya nje wakati wa kujamiiana?

---

Hapana, mara tu baada ya uume kuingia ndani ya kondomu, sio lazima kuendela kushika pete ya nje.

### Je! FC2 hupiga kelele wakati wa kujamiiana?

---

Hapana, FC2 ni kondomu laini na nyororo. Ukisikia kelele na ikakukera, ongeza kilainishi ama ndani au nje ya kondomu au moja kwa moja ndani ya uume. Pia jaribu kuingiza FC2 dakika chache kabla ya kujamiiana.

### Je nifanyeje, endapo wakati wa kujamiiana, pete ya nje itateleza ndani ya uke au kondomu itasukumwa ndani ya uke?

---

- Mwanaume anapaswa kuchomoa uume wake.
- Toa kondomu ya kike.
- Ingiza kondomu mpya ya FC2 ya kike.

### **Je! FC2 inaweza kutumika katika mikao tofauti ya kujamiiana?**

---

Ndio. Unaweza kujaribu mikao tofauti ya kujamiiana ukisharidhika kutumia FC2.

### **Je! FC2 inaweza kutumiwa tena?**

---

Hapana. Tumia FC2 mpya kwa kila tendo la kujamiiana.

### **Je! FC2 inaweza kupasuka wakati wa kujamiiana? ?**

---

Kama ilivyo kwa kondomu nyingine, umakini unahitajika kila siku wakati wa kuingiza kondomu ya kike. Usifungue pakiti na mkasi, kisu au meno yako, na shika kondomu kwa umakini kama una kucha ndefu. Kuchanika kwa FC2 kumeripotiwa chini ya 1%. Endapo FC2 itapasuka, itoe na weka kondomu mpya haraka.

### **Nifanyeje endapo uume utateleza kati ya kizuizi na kuta ya uke?**

---

- Mwanaume anapaswa kuchomoa uume wake haraka.
- Ni muhimu kushika pete ya nje wakati mwanaume (au mwanamke) anapoongoza uume wake ndani ya kondomu. Mara baada ya uume kuingia, sio lazima uendelee kushikiria pete ya nje.

### **Napaswa kufanyaje endapo kondomu inatoka nje sana nje ya uke (inaenda sambamba na uume)**

---

- Chomoa kondomu ya kike
- Ingiza mpya
- Tumia kilainishi zaidi ndani ya kondomu ya kike au kwenye uume moja kwa moja.

# 5

## FC2 pamoja na njia nyingine za kuzuia mimba

### Je! FC2 inaweza kutumiwa pamoja na njia nyingine za kuzuia mimba?

---

Ndio. FC2 inaweza kutumiwa pamoja na kidonge, sindano, lupu, kitanzi, na Vasektomi kutoa ulinzi dhidi ya magonjwa ya zinaa, ikiwemo VVU. FC2 haiwezi kutumiwa na njia ya diaphragm au ya Pete ya Mpira (NuvaRing) kwa sababu pete ya ndani ya FC2 inakaa kwenye sehemu sawa na pete ya vifaa hivyo vya kuzuia mimba.

### Je! FC2 na kondomu ya kiume vinaweza kutumika pamoja?

---

Hapana. Kamwe usitumie kondomu ya kiume na ya kike wakati mmoja. Kutumia kondomu hizo mbili kwa pamoja hakuongeza kinga bali huongeza nafasi ya moja au zote kupasuka.

It doesn't  
always have to  
hurt him.




# 6

## Jinsi ya kutumia kondomu ya kike ya FC2

Maelekezo haya yanaonyesha hatua kwa hatua jinsi ya kuingiza kondomu ya kike ya FC2 ndani ya uke. FC2 inaweza kuingizwa ama masaa machache au kabla tu ya kujamiiana.

Wakati FC2 inatumiwa kwa mara ya kwanza, watu wanaweza kuhitaji mazoezi ya kuingiza. FC2 inaweza kuingizwa na wanawake wenyewe lakini wenzi wao wanaweza pia kuwaingizia.



1


Kabla ya kufungua FC2 yako:

- Angalia tarehe ya kuisha muda wa matumizi ambayo imegongwa kwa muhuri mbele au kwenye upande wa pakiti ya FC2.
- Sambaza kilainishi ndani kuzunguka kwa kusugua pakiti kwa mikono yako.




2

- Ili kufungua pakiti, chana moja kwa moja kutoka kwenye mshale hapo juu kisha utoe kondomu.
- Usitumie mkasi, kisu au meno yako kufungua pakiti.




6

- Tumia upande wa pete ya ndani uliobonyezwa kusukuma FC2 kuingia ukeni mwako.
- Sogeza kidole cha kwanza au cha kati ndani ya kondomu na sukuma ndani ya uke wako mbali kadri uwezavyo, kwa kutumia pete ya ndani.
- Hakikisha kondomu haijazungushwa na imekaa vizuri dhidi ya kuta za uke wako.



7

Sehemu ndogo ya kondomu, ikiwemo pete ya nje, inakaa nje ya mwili wako na iko juu ya mashavu ya uke wako, kwa sehemu inalinda viungo vyako vya nje vya kujamiiana na kufunika sehemu ya chini ya uume wa mwenzi wako.




8

FC2 huingia ndani sambamba na uke wako na kuziba shingo ya kizazi. Shingo ya kizazi chako ni ndogo sana kiasi kwamba haiwezekani FC2 kupenya eneo hili.



3

Shika pete ya ndani kati ya kidole gumba chako na kidole cha mbele. Kisha bonyeza pembe za pete ya ndani pamoja ili kutengeneza uimara.



4

Unaweza kuingiza FC2 kwa njia nyingi tofauti. Tafuta mkao wa starehe. Hii inaweza kuwa kusimama, kukaa, kuchuchumaa au kulala chini.




5

Gusa mashavu ya nje ya uke wako na uyapanue.



9

Shika pete ya nje wakati mwenzi wako anapoingiza uume wake ndani ya kondomu. Uume wake ukishaingia ndani ya kondomu, sio lazima uendelea kushikilia pete ya nje. Kwa raha ya ziada unaweza kutaka kuongeza kilainishi zaidi ndani au nje ya FC2 au moja kwa moja kwenye uume wa mwenzi wako mara tu kondomu baada ya kondomu kuingizwa.



10

### Tafadhali zingatia!

Mwenzi wako anatakiwa kuchomoa uume wake mara moja endapo:

- Uume wake utaingia kati ya kondomu na kuta za uke. Hili likitokea unapaswa kurudisha pete ya nje katika nafasi yake kabla hajaingiza tena uume wake ndani ya kondomu.
- Pete ya nje itakua imesukumwa ndani ya uke wako. Hili likitokea unapaswa kutumia FC2 mpya.



11

Kutoa FC2, shika pete ya nje na izungushe kuzuia shahawa kumwagika. Ni vyema ufanye hivi kabla haujasimama. Vuta kondomu nje polepole, ifunge kwenye tishu au pakiti tupu, na kisha itupe kwenye ndoo ya uchafu.

# Kondomu ya kike ya FC2 Kwa tendo la kujamiiana lenye furaha na salama



**Unapoongea na watu kuhusu kondomu ya kike ya FC2 kwa mara ya kwanza, mara nyingi huwa na maswali mengi juu yake. Na wanapoanza kutumia FC2, wanaweza kuwa na maswali mengi zaidi. Chapisho hili linakupa majibu ya maswali yote hayo.**

[www.fc2femalecondom.com](http://www.fc2femalecondom.com) | [info@fc2femalecondom.com](mailto:info@fc2femalecondom.com)

f @FemaleCondomFC2  
t @FC2FemaleCondom  
v FC2FemaleCondom

Kondomu ya Kike ya FC2 inatengenezwa  
na The Female Health Company (FHC).  
Chicago USA/London UK/Malaysia